**OFISI YA RAIS**
**TAWALA ZA MKOA NA SERIKALI ZA MTAA**
**HALMASHAURI YA WILAYA YA ULANGA**

**Namba za simu………………………….**
**Mkuu wa Shule.0753046896**
**Makamu Mkuu wa shule .0767212868**
**Matron/Patron.0764056886/0767114043**

**SHULE YA SEKONDARI NAWENGE.**
S.L. P. 78,
**MAHENGE/ULANGA-MOROGORO**.
22/5/2025

.

**MZAZI /MLEZI WA MWANAFUNZI……………………………………………………**
**S.L.P……………………………………………………………………………………**
**…………………………………………………………………………………………..**

**YAH: MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO KATIKA SHULE YA SEKONDARI NAWENGE HALMASHAURI YA ULANGA MKOA WA MOROGORO MWAKA 2025**

1. Nafurahi kukutaarifu kuwa mwanao amechaguliwa kujiunga na kidato cha tano katika shule hii mwaka 2025 na atasoma tahasusi ya **HGL, HGK, CBG na HGFa.** Uongozi wa Shule unachukua nafasi hii kukupongeza na kukukaribisha
   Shule ya Sekondari NAWENGE ipo umbali wa kilomita 2 kutoka Mahenge Mjini Makao makuu ya wilaya mji wa MAHENGE usafiri wa basi kutoka Dar es salaam au Morogoro kwa basi la moja kwa moja mpaka mahenge kwa kutumia mabasi ya ADINAS, MBEKENYELA, KIDILO, ZEELAND, EFRA, AG SAFARI unapatikana .
   Muhula wa Masomo unaanza mwezi julai mwanafunzi anatakiwa kuripoti shuleni.

**2.Mambo Muhimu ya Kuzingatia:-**

2.1 **Sare za shule**.

i. Sare ya shule hii ni rangi ya kijivu mpauko cotton,sketi mbili za rinda box ndefu hadi chini kwa wasichana na wavulana suruali mbili upana wa sentimeta 16 chini zenye turn up.
   **Tanbihi; kuepuka kukosea rangi unaweza kuzipata shuleni.**
ii. Shati mbili nyeupe za mikono mirefu (tomato). Nembo ya shule inapatikana hapa shuleni
iii. Viatu vya ngozi nyeusi jozi mbili vya kamba na vyenye kisigino kifupi.**Usije na viatu visivyo vya kamba.**
iv. Tai yenye rangi ya maroon yenye mistari mieupe.(inapatika shuleni kwa tshs. 6000/=).
v. Soksi jozi 02 nyeupe ndefu.
vi. Sweta 02 za kijivu.(unaweza kuzipata shuleni).
vii. T-Shirt 02 za kushindia baada ya masomo rangi ya summer blue na yenye kola (form six) (Zenye nembo ya shule zinapatikana shuleni kwa shilingi 18,000/=).
viii. Sketi 02 za rangi nyeusi (Rinda box) ndefu mpaka chini kwa wasichana na suruali nyeusi kwa wavulana. Upana wa cm 16 zenye turn up za kushindia
ix. Track suti NZITO **rangi** ya kijivu(Addidas, Apple etc)
x. Mashuka mawili, rangi ya pinki kwa wasichana na light bluu kwa wavulana
xi. Pullneck **nzito** mbili za kijivu .(unaweza kuzipata shuleni).
xii. -Hijabu kwa wasichana wakiislamu watakaopenda kuvaa hivyo. Rangi ya hijab ni nyeupe kwa darasani na bluu kwa kushindia. Isiyo na urembo**(NB; usije na mitandio).**
xiii. Pasi ya mkaa ya kunyoshea nguo **isiwe** ya umeme.

N.B.**vifaa tajwa hapo juu vinapatikana karibu na mazingira ya shule**

**2.2** Michango ya shule

a) Michango inayotakiwa kulipwa na kila mzazi ni: -

| Na | Aina ya mchango | Kiasi |
|---|---|---|
| 1 | Mchango wa uendeshaji wa shule | 65 000/= |
| 2 | tahadhari | 5, 000/= |
| 3 | Nembo | 5, 000/= |
| 4 | Kitambulisho cha shule | 5. 000/= |
| | **Jumla** | 80,000/= |

N; B Fedha hizo zote ziingizwe kwenye akaunti ya shule ya **NMB**, **NAWENGE SECONDARY SCHOOL No.21901000021**, katika tawi lolote la NMB. Mwanafunzi ajapo shuleni aje na "**Bank Pay in Slip".** Kumbuka kuandika jina la mwanafunzi kwenye pay in slip. Mwanafunzi ambaye hatakuja na Bank Pay in Slip hatapokelewa.

Kwa wale wanaolipiwa na wafadhili wakumbuke kuleta uthibitisho wa maandishi yanayoonesha aina ya malipo watakayolipiwa na yatalipwa lini.

Mzazi unaombwa kumtengenezea mtoto bima ya afya (NHIF) aje nayo ama kumfanyia utaratibu wa CHIF (6000/=) atakapofika shuleni kwa kuwasiliana na mwalimu wa malezi ili aunganishwe na Hospital ya Wilaya.

Pia mtoto anatakiwa aje na Tshs10000/= kwa ajili ya Matron/Patron wa shule.

**2.3 Vifaa vya malazi,chakula na usafi.**

i. Unatakiwa kuwa na jembe moja lenye mpini, Hard broom, pamoja na kwanja moja kwaajili ya kufanyia usafi .
ii. mifagio 02 mmoja kwa ajili ya kufagia nje (chelewa yenye mpini), na mwingine kwa ajili ya kufagia ndani soft bloom kwa wote.
iii. Squeezer (mopper/drier) kwa HGL na HGK.
iv. Reki yenye mpini kwa CBG.
v. Toilet brush kwa HGFa
vi. Sabuni ya unga (AZANIA/TOSS/KLEENSOFT) ndoo ndogo 1.
vii. Godoro la nchi $2^{1}/_{2}$ x6.
viii. Sahani, kikombe na kijiko kwa ajili ya chakula viwe vya udongo/mifupa
ix. Ndoo 02 ndogo za plastic zenye mifuniko.
x. Blanket moja nzito kuna baridi kipindi kirefu cha mwaka
xi. Gum boot (rain boot).

**2.4 Vifaa vya masomo**.

i. Daftari 8 kubwa kwa kuanzia (Counter Book QUIRE 3).
ii. Daftari 10 ndogo na karatasi za kutosha kwa ajili ya majaribio ya mara kwa mara.
iii. Kalamu ya wino- bluu au nyeusi.
iv. Mfuko wa vitabu (School bag).
v. Ream mbili **(A4)** (02) kwa mwaka.
vi. Vitabu vya masomo utakayo yasoma ni muhimu,orodha imeambatanishwa.
vii. Koti JEUPE LA MAABARA, Dissecting kit na calculator (scientific Casio fx 991) Kwa CBG.

viii. File, Graph pad, mathematical set kwa wote.

2.**5 Vifaa vya Michezo**.

Unatakiwa kuwa na vifaa vya michezo vifuatavyo, ili kuvitumia wakati wa michezo mbalimbali hapa shuleni na nje ya shule. Michezo kwetu ni muhimu kila mmoja kushiriki.

i. Viatu vya michezo (RABA ZA MICHEZO)
ii. Jezi za rangi nyekundu (ARSENAL) kwa wote (NB usije na jezi tofauti).

2.6. **Vifaa vingine**

Unatakiwa kuja na vifaa vya matumizi ya kila siku kama vile; taulo,dawa ya meno, sabuni za kuogea na kufulia, mafuta ya kupaka, taulo za kike kwa wasichana, ndala za kuogea n.k. Ni vyema pia ukaja na sanduku la mbao au la bati (tranka) kwaajili ya kutunzia vifaa vyako. Kumbuka nguo za kiraia ambazo si sare (uniform) za shule na ambazo hazikutajwa katika fomu hii haziruhusiwi kuvaliwa shuleni.***Mwanafunzi haruhusiwi kuja na vipodozi, pafyumu (spray) na vipodozi vyote vya kujiremba na kuchubua ngozi.***

***NB. Mtoto anatakiwa kuwa na pesa kidogo kwa ajili yamatumizi binafsi (pocket money).***

**3.0. SHERIA NA KANUNI ZA SHULE.**

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa sheria ya Elimu Na.25 ya mwaka 1978 na kama ilivyorekebishwa kwa sheria Na.10 ya mwaka 1995.Aidha inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu,Sayansi na Teknolojia yenye dhamana ya elimu nchini na ofisi ya Rais-TAMISEMI yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji wa elimu nchini. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yanafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shuleni.
Sheria na kanuni za shule zinatungwa kufuatana na maadili ya Taifa letu.Lengo ni kutoa mwongozo na msaada kwamwanafunzi ambaye anatarajiwa awe raia na Mzalendo wa Jamuhuri yaMuungano wa Tanzania. Utii wa sheria za shule ni utii wa sheria za taifa letu. Shule imepewa jukumu la kulea na kuelimisha vijana ili baadae wawe raia wema wa Taifa hili. Sharti mwanafunzi kufuata kanuni na sheria za shule. Zifuatazo ni sheria za shule na kila mwanafunzi anatakiwa aziheshimu na kuzizingatia ipasavyo:-

1. Mwanafunzi sharti awaheshimu walimu na wafanyakazi wote wa shule ambao ni walezi wake. Ajiepushe na lugha chafu, utovu wa nidhamu kwa walezi hawa. Inampasa mwanafunzi kusimama sawa anapomwona mwalimu au mfanyakazi na mgeni yeyote ambaye anamzidi umri na kumwamkia ipasavyo.
2. Ni kosa kubwa kwa mwanafunzi kukataa kufanya kazi za shule,au adhabu ya mwalimu au kiongozi yeyote yule wa wanafunzi aliyechaguliwa kwa mujibu wa sheria.
3. Kila mwanafunzi ni lazima ahudhurie vipindi vyote vya darasani na nje alivyopangiwa kwa wakati uliopangwa na afanye mitihani, majaribio na mazoezi yote yatakayotolewa ndani na nje ya shule. Ni kosa kubwa kukosa vipindi na kutofanya majaribio, mazoezi na mitihani mbalimbali bila sababu maalum.

4. Ni marufuku mwanafunzi kutoka nje ya mipaka ya shule isipokuwa kwa kibali maalum cha Mkuu wa shule, kila mwanafunzi atawajibika kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelezo juu ya kuwepo ndani na nje ya mipaka ya shule wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii.
5. Kila mwanafunzi atalazimika kuzingatia ratiba ya siku nzima na kuitekeleza “Daily Routine”
6. Kila mwanafunzi analazimika kuvaa sare ya shule wakati wote.
7. Kila mwanafunzi atalazimika kuhudhuria maandalio ya jioni na ya siku za mwisho wa wiki kama yalivyopangwa (Preparation).
8. Kila mwanafnzi lazima azingatie kuwa haruhusiwi kwenda kwenye nyumba ya mtumishi yeyote pasipo ruhusa wakati wote akiwa mwanafunzi.

9. Ni lazima mwanafunzi ajiepushe na makosa ambayo yanaweza kusababisha afukuzwe shule. Makosa hayo ni haya yafuatayo;

i. Wizi
ii. Kutohudhuria masomo kwa zaidi ya siku 90 bila taarifa/ utoro
iii. Uasherati, Ubakaji, uhusiano wa jinsia moja, kuoa au kuolewa
iv. Ulevi au unywaji wa pombe na matumizi ya madawa ya kulevya
v. Uvutaji wa sigara
vi. Kupigana mwanafunzi kwa mwanafunzi, kumpiga mwalimu au na mtu yeyote Yule.
vii. Kusuka au kunyoa nywele kwa mtindo usiokubalika. Wanafunzi wote wanatakiwa kuwa na nywele fupi wakati wote wawapo shuleni.
viii. Kufuga ndevu
ix. Kuharibu kwa makusudi mali ya umma, endapo ataharibu Mali atalazimika kulipa.
x. Kujihusisha na mahusiano ya kimapenzi ndani na nje ya shule kipindi chote uwapo shuleni.
xi. Kudharau Bendera ya Taifa na picha za viongozi wakuu wa Serikali.
xii. Kupata mimba au Kutoa au kushiriki kutoa mimba.
xiii. Kusababisha mimba au kumpa mimba msichana ndani na nje ya shule.
xiv. Kushiriki matendo ya uhalifu, siasa na matendo yoyote yale yanayovunja sheria za nchi(Makosa ya jinai)

xv. Kugoma, kuhamasisha mgomo, kuongoza au kuvuruga amani na usalama wa watu.
xvi. Kutoa lugha chafu kwa wanafunzi wenzake, walimu/ walezi na jamii kwa ujumla
xvii. Kutembelea majumba ya starehe na nyumba za kulala Wageni.
xviii. Airuhusiwa kwa mwanafunzi kumiliki, kukutwa, au kutumia simu ya mkononi katika mazingira yeyote , akiwa ndani au nje ya shule.
xix. Mwanafunzi haruhusiwi kubadili dini wala kumshawishi mwanafunzi mwenzake kubadili dini wawapo shuleni.
xx. Kufanya jaribio lolote la kujiua, au kutishia kujiua kama kunywa sumu.

**MUHIMU**

i) Mwanafunzi awapo shuleni atatakiwa kulala kwenye bweni alilopangiwa na kitanda alichopangiwa. Ni marufuku mwanafunzi kulala kitanda kimoja na mwenzake au kuishi kwenye bweni ambaalo hakupangiwa.
ii) Mwanafunzi ataruhusiwa kurudi nyumbani kwa ruhusa na kibali maalumu toka kwa mkuu wa shule( msiba au ugonjwa).
iii) Mwanafunzi hapaswi kuja na simu shulenikwa na mna yoyote ile na hakuna mtumishi anayeruhusiwa kutunza simu ya mwanafunzi.
iv) **KWA MATUMIZI YA SIMU ITATUMIKA SIMU KATIKA OFISI YA MALEZI TU.**

**SHULE YA SEKONDARI NAWENGE**
**FOMU YA KUANDIKISHWA SHULE**

(Ijazwe kwa herufi kubwa na irejeshwe kwa mkuu wa shule)

1. Jina kamili………………………………………………………………………………………………………
   Tarehe ya kuzaliwa…………………… Wilaya………………………Mkoa…………………………….
   Taifa………………………Dini:RC/Anglican/Lutheran/Muslim/Pentecoste/n. k………………….
   Shuleya sekondari unayotoka……………………………………………………………………………
2. Jina kamili laBaba/Mama/Mlezi…………………………………………………………………………
   Anwani yake ……………………………………………………………………………………………….
   Kazi ya Baba/Mama/Mlezi……………………………………………………………………………….
   Namba ya simu……………………………………………………………………………………………
   Barua pepe…………………………………………………………………………………………….

**AHADI YA MWANAFUNZI**.

a) Mimi………………………………………………………………nimeyasoma na kuyaelewa maelekezo yote ambayo ni pamoja na sheria za shule na kanuni za shule na nimekubali kuingia kidato cha TANO katika shule ya sekondari NAWENGE kuanzia tarehe……………………hadi nitakapomaliza kidato cha SITA.
b) Kwahiyo naahidi kwamba:-
   i. Nitazitii sheria zote za shule na kutimiza mambo yote muhimu yaliyotajwa
   ii. Sitashiriki katika vitendo vya hujuma wala vitendo ambavyo vitakuwa kinyume na uongozi wa shule na serikali ya Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania.Kama kushiriki migomo, fujo,makosa ya jinai n.k
   iii. Nitatunza mali za umma ambayo ni pamoja na majengo, samani, vitabu n.k
   iv. Nitatimiza malengo ya kitaaluma ya shule kwa kupata daraja la kwanza na la pili.

Tarehe………………………Sahihi ya Mwanafunzi…………………………………

**<u>AHADI YA MZAZI/MLEZI</u>.**

Mimi………………………………………………………………………ambaye ni Mzazi /Mlezi wa Mwanafunzi……………………………………………………………………………

Ninaahidi kwamba :-

1.Nitashirikiana na uongozi wa Shule,Walimu na Watumishi wasio walimu katika kuhakikisha mwanangu anatii sheria na kanuni za Shule ya Sekondari NAWENGE. Iwapo atashindwa kutii sheria hizo, nitalazimika kukubaliana na adhabu itakayotolewa na uongozi wa shule.

2.Nitafanya kila niwezalo kumwezesha mwanangu kusoma kwa kulipa ada na michango mingine kama ilivyoelekezwa na shule.

Sahihi……………………………………………………..
Tarehe…………………………………………………….
Namba ya simu……………………………………………

**ULANGA DISTRICT COUNCIL**
**NAWENGE SECONDARY SCHOOL**

## MEDICAL EXAMINATION FORM

(Ijazwe na mganga mkuu wa hospitali ya serikali)

To be completed by medical Officer in respect of NAWENGE Secondary School Student (Entrant).

1. Full name of student………………………………………………………………………………….
2. Sex………………………………………… Age…………………………………………………………
3. HGB Test……………………………………………………………………………………………….
4. Stool………………………………………………………………………………………………………
5. Urine
   Micro………………………………………………………………………………………………………
6. T.B
   Test………………………………………………………………………………………………………
7. Eye Examination………………………………………………………………………………………
8. E.N.T…………………………………………………………………………………………………….
9. Chest………………………………………………………………………………………………………
10. Abdomen………………………………………………………………………………………………

**ADDITIONAL INFORMATION**.

Physical Defects or Impairment, Infections, Chronic or Hereditary (family) diseases.

………………………………………………………………………………………………………
………………………………………………………………………………………………………
………………………………………………………………………………………………………
………………………………………………………………………………………………………
…………………………………………………

I certify that I have examined the above student and consider that* he/she is physically/not physically fit for further studies.

NAME………………………………………………………………………..
SIGNATURE……………………………………………………………….

DATE……………………………………………………………………….
OFFICIAL STAMP

**ORODHA YA BAADHI YA VITABU VYA MASOMO**
**JIOGRAFIA**

1. Msabila , D. T. (2019) (A Comprehensive Approach to Physical Geography
2. Kamili, Z (Current Edition) Practical Geography Alive
3. Geography 1 reviews
4. Human and Economic Geography. By DT Msabila.

**HISTORIA**

1. Kato A.K (2014)
   Mastermy History. History 1 and history 2.
2. Zisti Kamili – Advanced History Part One Alive
3. Advanced level Histiry part two.
4. Contemporary history events –history two by mwl shibitali
5. Essential in Advanced level history paper 2 and paper 1 by Saleh Yassin

**KISWAHILI**

1. Nadharia Ya Kiswahili 1- Kidato Cha Tano na Sita
2. Nadharia Ya Kishwahili 2- Kidato Cha Tano na Sita

3 . Vitabu vya riwaya,ushairi na tamthilia- Kimbunga,Kivuli Kinaishi,Kufikirika,Vuta Nikuvute,Mfadhili,Usiku Utakapokwisha,Morani,Nguzo Mama,Ukingo Wa Thim,Chungu Tamu,Fungate Ya Uhuru,Mapenzi Bora

3. DAFINI YA LUGHA.
4. Kiswahili kidato cha tano na sita Sarufi.
5. Kiswahili nadharia ya lugha.

**ENGLISH LANGUAGE**

**A) English language one**

1. **Ndambo ,S.G &Kinunda,J.E () English language 1 for form five and form six**
2. **ASheli ,N () Advanced level english language 1**
3. Recommended English Language One Text Book For A- Level Student ( By Paschal Salawi)
4. Advanced leaners oxford Dictionary English To English

**B) English language two**

**NOVELS**

1. His Excellence Head Of State
2. ,A Man Of The People,
3. The Beautiful Ones Are Not Yet Born,
4. Encounters from Africa

**PLAYS**

1.An Enemy Of The People

2.Betrayal in the city

3.I will marry when I want

POETRY

Selected Poem from East Africa

Wonderful Surgeon

**BIOLOGY**
1. Biological Science
2. Understanding Biology

**CHEMISTRY**
1. Advanced Chemistry By Ramsdem
2. Inorganic Chemistry Part I Na Part 2 (Tie)
3. Chemistry For Secondary Schools Fv ,F vi By T.I.E
4. Physical chemistry and organic chemistry E.N Ramsdem
5. Conceptual organic chemistry S. Chandi
6. Advanced level Inorganic Chemistry Part I and II
7. Environmental And Soil Chemistry.

**GENERAL STUDIES.**
1. General Studies for Advanced Level Certificates Form

**BASIC APPLIED MATHEMATICS**
1. Basic applied mathematics for sec schools form v and form vi (TIE)

**Tafadhali soma kwa makini maelezo/ maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu.**

Uongozi wa shule unakutakia maandalizi mema na safari njema ya kuja hapa.

MWL MAGRETG D. LISSA.
MKUU WA SHULE.

KARIBU SANA KATIKA SHULE HII

Saini ya Mkuu wa Shule:
Jina la Mkuuwa shule : MAGRETH D. LISSA.
Mhuri wa Mkuu wa SHULE:

N.B:**Kwa siku za hivi karibuni kumekuwa na utapeli (wizi kwa njia ya mtandao).Baadhi ya wazazi wamekuwa wakitumiwa ujumbe mfupi au kupigiwa simu na watu wanaojitambulisha kama walimu na kuwafahamisha kuwa mtoto wa mzazi husika ambaye ni mwanafunzi ni mgonjwa na yupo mahututi hivyo mzazi atume pesa.TAFADHALI UPATAPO UJUMBE WOWOTE KUHUSU MWANAFUNZI/MTOTO WAKO USITUME CHOCHOTE,NI VEMA UKAWASILIANA NA UONGOZI WA SHULE KUPATA UKWELI WA TAARIFA HUSIKA KWA NAMBA ZIFUATAZO:**

- **MKUU WA SHULE . 0753046896**
- **MAKAMU MKUU WA SHULE 0767212868**
- **MWANDAMIZI TAALUMA 0767114043**
- **MWANDAMIZI MALEZI.0764056886 .**

**MHIMU; kwa msaada wa kupata mahitaji yote ya shule yaani vifaa na sare shule wasiliana na ofisi ya malezi kupitia no. 0758209920/0658209920.**